JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2022

## UALIMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2022

## 610 UALIMU

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


**DIBAJI ........ IV**

**1.0 UTANGULIZI ........ 1**

**2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI 3**

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ........ 3
2.1.1 Swali la 1: Utafiti wa Kielimu ........ 3
2.1.2 Swali la 2: Nadharia za Kujifunza ........ 5
2.1.3 Swali la 3: Ufundishaji ........ 8
2.1.4 Swali la 4: Mtaala ........ 11
2.1.5 Swali la 5: Upimaji katika Elimu ........ 15
2.1.6 Swali la 6: Utafiti wa Kielimu ........ 17
2.1.7 Swali la 7: Tathmini katika Elimu ........ 20
2.1.8 Swali la 8: Maendeleo ya Elimu Tanzania ........ 23
2.1.9 Swali la 9: Elimu ya Watu Wazima ........ 25
2.1.10 Swali la 10: Uongozi wa Elimu Tanzania ........ 28
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA ........ 31
2.2.1 Swali la 11: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto ........ 31
2.2.2 Swali la 12: Ufundishaji ........ 38
2.2.3 Swali la 13: Upimaji katika Elimu ........ 44
2.2.4 Swali la 14: Elimu ya Watu Wazima ........ 51

**3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........ 57**

**4.0 HITIMISHO ........ 57**

**5.0 MAPENDEKEZO ........ 58**

***KIAMBATISHO CHA PEKEE* ........ 59**

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limetayarisha taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa cheti daraja la A katika somo la Ualimu mwaka 2022. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani au vibaya katika mtihani huu. Kwa ujumla, ufaulu katika somo la Ualimu ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa walitambua mahitaji ya swali, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika, walielewa vizuri dhana mbalimbali zilizotahiniwa, walikuwa na uwezo wa kujibu maswali kulingna na nyanja husika na walikuwa na ujuzi wa kutosha katika uandishi wa insha. Vilevile, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu wa wastani, watahiniwa walitoa hoja chache kuliko matakwa ya swali husika na wengine walirudia hoja moja kwa namna tofauti.

Hata hivyo, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Ualimu na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika sehemu za utangulizi na hitimisho hususan katika maswali ya insha. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali waliyojibu unatoa picha halisi ya mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu katika vyuo vya Ualimu Tanzania.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanachuo kutumia mbinu muafaka ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Maboresho hayo yatasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Wakufunzi na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.



Athumani S. Amasi

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Ualimu kwa watahiniwa wa ngazi ya Astashahada uliofanyika mwezi Mei, 2022, uliandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo la Ualimu wa mwaka 2009 ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi. Mtihani huo ulikuwa na maswali kumi na nne (14), ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi, na kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B ilikuwa na maswali manne (04) ya insha ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15).

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika somo la Ualimu kwa mwaka 2022 kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 3,244 (99.85%) walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri. Kiwango hiki cha ufaulu kimeshuka ikilinganishwa na mwaka 2021 kama inavyoonekana katika jedwali la pekee.

| Mwaka | Watahiniwa Waliofanya | Asilimia ya Watahiniwa Waliofaulu (%) | Madaraja | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | A | B | C | D | F |
| 2021 | 2,950 | 100 | 40 | 1,037 | 1,743 | 101 | 0 |
| 2022 | 3,272 | 99.85 | 22 | 804 | 2,272 | 146 | 5 |

Jedwali la pekee linaonesha kuwa, asilimia 99.85 ya watahiniwa walifaulu kwa mwaka 2022, na ufaulu ulishuka kwa asilimia 0.15 ikilinganishwa na mwaka 2021.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni ufaulu mzuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, kiwango cha ufaulu kwa kila swali katika sehemu A ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata alama 3 na 4; kiwango cha *wastani* alama 2 na 2.5 na kiwango *hafifu* alama 0 na 1.5. Kwa maswali ya sehemu B, kiwango cha ufaulu katika kila swali ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata 10.5 na 15; kiwango cha *wastani* alama 6 na 10 na kiwango *hafifu* alama 0 na 5.5.

Katika kufanya uchambuzi na kutafsiri ufaulu wa watahiniwa, chati zimetumika ili kufafanua ufaulu husika. Rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa somo la Ualimu. Sampuli za majibu ya watahiniwa yameambatishwa ili kuonesha majibu waliyofanya vibaya na waliyofanya vizuri. Aidha, taarifa inaonesha sababu zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kupata au kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa mada

zilizotahiniwa. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu kwa mada hizo ili kuongeza ufaulu wa watahiniwa katika mitihani yao.


## 2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Maswali katika sehemu A yalitoka katika mada tisa (9) ambazo ni*: Upimaji Katika Elimu, Nadharia za Kujifunza, Ufundishaji, Mtaala, Utafiti wa Kielimu*, *Tathmini katika Elimu*, *Maendeleo ya Elimu Tanzania*, *Elimu ya Watu Wazima* na *Uongozi wa Elimu Tanzania*. Kila swali lilikuwa na alama nne (4) hivyo kufanya jumla ya alama arobaini (40).

#### 2.1.1 Swali la 1: Utafiti wa Kielimu


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuorodhesha mambo manne atakayozingatia wakati wa kukusanya taarifa za wanafunzi wa Darasa la Pili katika shule yake. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwa kuwa watahiniwa 52 (1.6%) walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




***Chati Na. 1:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa watahiniwa wengi (98.4%) walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 1.4 alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa wachache (0.2%) alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, wengi wao (98.4%) walipata alama 0 hadi 1.5 kwa sababu hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu yaliyo tofauti. Kati yao, watahiniwa wengi (92.1%) walipata sifuri kwani badala ya kuorodhesha mambo ya kuzingatia wakati wa kukusanya taarifa za wanafunzi, wengi wao waliorodhesha taarifa ambazo zinatakiwa kukusanywa kama vile: *umri wa wanafunzi, mahudhurio darasani, tabia na mwenendo wa mwanafunzi, ushirikiano na wenzake, idadi ya wasichana na wavulana* na *maendeleo kitaaluma*. Mtahiniwa mmojawapo aliorodhesha mambo ya kuzingatia kuwa ni: *kuzingatia uwepo wa daftari la mahudhurio, taarifa kutoka kwenye orodha hakiki, taarifa kutoka kwenye shajara* na *kuwa na jedwali la utahini.* Aidha, mtahiniwa mwingine aliorodhesha mambo hayo kuwa ni: *kupitia daftari la mahudhurio, kufanya uchunguzi mwenyewe, kupitia wanafunzi wenyewe* na *kupitia kwa mwalimu wa darasa hilo.* Watahiniwa walitakiwa kuorodhesha mambo ya kuzingatia ambayo ni: *aina mahsusi ya data za kukusanya, kuandaa zana za kukusanyia taarifa hizo, utaratibu na njia zilizochaguliwa za kukusanya taarifa* na *kurekodi taarifa zinazokusanywa.* Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili.


1 i) Ufundishaji wa mahiri
ii) jinsia
iii) Waliosajiliwa
iv) Waliohudhuria


**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa aliorodhesha baadhi ya taarifa zinazoweza kukusanywa kutoka kwa wanafunzi badala ya kuorodhesha mambo ya kuzingatia wakati wa kukusanya taarifa za wanafunzi.

Takwimu zinaonesha pia kuwa, asilimia 1.4 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao, hivyo walishindwa kupata alama zote nne. Wengi wa watahiniwa katika kundi hili walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi; na wengine walitoa majibu pungufu hivyo walishindwa kupata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu sahihi kama: *aina mahususi ya data* na

*zana na njia za kukusanyia data*. Pia alijumuisha na jibu lisilo sahihi ambalo ni, *kutafsiri data na kuwasilisha matokeo*. Aidha, aliandika jibu lingine la *kufanya uchunguzi wa data za kukusanya* ambalo linafanana na jibu la awali la *kuchunguza aina mahususi ya data za kukusanya*.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, wachache kati yao (0.2%) walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa katika kundi hili walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Utafiti wa Kielimu*, hususan kipengele cha *Hatua za Kufanya Utafiti wa Kielimu*. Mtahiniwa mmoja aliyepata alama zote nne alielewa vema matakwa ya swali, hivyo alitoa majibu sahihi kama vile: *aina mahsusi ya data za kukusanya, kuandaa zana za kukusanyia taarifa hizo, utaratibu na njia zilizochaguliwa za kukusanya taarifa* na *kurekodi taarifa zinazokusanywa*. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 1.



i) Aina Mahususi ya data au taarifa na kukusanya
ii) Kuandaa zana za kukusanyia data au taarifa. Mfano Viudadisi.
iii) Kuzingatia kanuni na taratibu za kukusanya data au taarifa
iv) Kurekodi matokeo ya data au taarifa.

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa aliorodhesha mambo manne atakayozingatia wakati wa kukusanya taarifa za wanafunzi wa Darasa la Pili katika shule yake.

### 2.1.2 Swali la 2: Nadharia za Kujifunza


Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Katika kipengele (a), mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi maana ya uhawilisho hasi wa Maarifa. Katika kipengele (b), mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa kifupi mambo matatu yanayosababisha uhawilisho hasi. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa kuwa watahiniwa 555 (17%) walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.




***Chati Na. 2:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, watahiniwa wengi (83%) walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 15.3 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 1.7 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kati ya asilimia 83 ya watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5, asilimia 10.6 walipata sifuri. Watahiniwa hao walikosa maarifa yanayohusu uhawilisho hasi na mambo yanayosababisha uhawilisho hasi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizosahihi kama vile: *uhawilisho hasi ni kitendo cha kuingiliana kwa maarifa yale ya zamani na yale ya sasa.* Alifafanua pia mambo yanayosababisha uhawilisho hasi kuwa ni: *mwalimu kuwa mkali, mwalimu kuto kujiandaa* na *wanafunzi kulichukia somo*. Mtahiniwa mwingine alieleza kuwa uhawilisho hasi ni *utoaji wa maarifa wenye kutaka kutoa adhabu kwa Mtendaji,* na mambo yanayosababisha uhawilisho hasi kuwa ni: *kutofanya maagizo yanayotolewa na mwalimu, kutotii sheria* na *tabia.* Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali la 2.



2

a. Uhawilisho hasi wa maarifa
Ni ufundishaji /ujifunzaji ulioko nje ya lengo mahususi na usiokuwa na maana katika ujifunzaji.


b. I. kutozingatia kutumia malengo ya mtaala
II. kufundisha bila kuandaa Azimio la kazi au Andalio la Somo
III. kufundisha bila kutumia mbinu za Ufundishaji wala Zana.

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa aliandika sababu zinazohusu kutofikiwa kwa malengo ya somo, badala ya kutoa maana ya uhawilisho hasi na kufafanua mambo yanayosababisha uhawilisho hasi.

Kwa upande mwingine, asilimia 15.3 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Wengine walifafanua sababu pungufu au zisizojitosheleza, hivyo walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana sahihi ya uhawilisho hasi kuwa ni: *maarifa ya awali huzuia ujifunzaji wa maarifa mapya*. Alitoa pia hoja moja sahihi ambayo ni *kuzidi kufanana kwa mambo*. Kwa upande mwingine, alitoa hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni: *muda* na *uanzaji wa maarifa mapya*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 1.7 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa wachache (0.1%) walipata alama zote nne kwa sababu walitoa maana ya uhawilisho hasi na kufafanua mambo yanayosababisha uhawilisho hasi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya *uhawilisho hasi*, hivyo walitoa majibu sahihi kama vile: *kufanana kwa mambo kukizidi, kushindwa kumudu vema maarifa ya awali* na *ujumlishaji wa mambo mawili bila kujua undani wake.* Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



2 a) Uhawilisho hasi?
Ni kitendo au ni hali inayopelekea
Mtu maarifa aliyonayo kuzuia ujifu
nzaji wa maarifa mapya.
b) Mambo kufafana kupita kiasi?
i) Kujifunza kitu kipya kabla ya kuelewa kile ali
chotangulia kujifunza. Mfano kama ni kipengele
fulani kinaendana na kipengele anachotaka
kujifunza lakini kipengele kilichopita hakukielewa
husababisha Uhawilisho hasi.
iii) Kufanya jambo bila kulielewa Undani wake
linataka nini.

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa alieleza maana ya uhawilisho hasi na kufafanua mambo yanayosababisha uhawilisho hasi kwa usahihi.

### 2.1.3 Swali la 3: Ufundishaji


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa faida mbili na hasara mbili za mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla ufaulu ulikuwa hafifu kwa kuwa watahiniwa 528 (16.1%) walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




***Chati Na. 3:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, watahiniwa wengi (83.9%) walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 13.2 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 2.9 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa hao unaonesha kuwa, asilimia 83.9 walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa waliopata sifuri (24.2%) hawakuwa na maarifa kuhusu mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja, hivyo waliandika majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa faida zisizosahihi kama vile: *haimchoshi mwanafunzi katika ujifunzaji* na *husoma vitu vingi kwa wakati mmoja.* Pia, alitoa hasara zisizosahihi ambazo ni: *kutofikia malengo mahususi ya mwalimu* na *kutomaliza mada*. Mtahiniwa mwingine pia alieleza kuwa faida ni; *kutunza kumbukumbu kwa muda mrefu* na *kupata muda wa kufanya marudio.* Vilevile, alitoa hasara ambazo ni: *kusoma vitu vichache kwa muda mrefu* na *kusahau kwa haraka maarifa yaliyopita*. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hili.


faida
(i) Husaidia kuwa na mpangilio mzuri wa maudhui
(ii) Husaidia kujenga kumbukumbu ya muda mrefu


Hasara
(i) Kutumia muda mrefu kukamilisha malengo ya somo.
(ii) Kushindwa kumaliza mada kwa muda husika ulio pangwa.

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa alielezea mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja kama mbinu ya kufundishia, badala ya kutoa faida na hasara za mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja.

Aidha, asilimia 13.2 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hawa walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao. Kwa mfano, kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kutoa majibu pungufu ya yaliyohitajika kwenye swali na kutoa hoja zenye usahihi kidogo, hivyo walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alieleza kuwa faida ni: *mwalimu kupata uzoefu wa kufundisha*. Alieleza faida nyingine ambayo ni dhaifu kuwa: *mwalimu tarajali kujijengea ujasiri*. Mtahiniwa huyu aliendelea kueleza hasara zenye madhaifu kuwa ni: *muda mfupi* na *kutokupata uzoefu wa kutosha*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha.

Vilevile, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 2.9 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa wachache (0.2%) walipata alama zote nne kwa sababu walikua na maarifa ya kutosha katika mada ya *Ufundishaji*. Watahiniwa hao walitoa faida mbili na hasara mbili za mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika faida ambazo ni: *haina gharama kubwa* na *inatoa nafasi ya kufanya mazoezi kwenye mazingira halisi*. Pia alieleza hasara kuwa ni: *muda mfupi wa maandalizi kwa mwalimu mwanafunzi* na *wanafunzi wa shule husika kukatishwakatishwa mtririko wa somo husika*. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


3 faida ya mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja
i/ Humsaidia mwalimu tarajali kujijengea uzoefu
katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji
ii/ Humsaidia mwalimu tarajali kujitathmini ma
funzo aliyopata kupitia ufundishaji huo


Hasara zake
i/ Huwafanya wanafunzi kufundishwa kwa m
tiririko usiofaa
ii/ Huathiri vipindi vingine

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alitoa faida mbili na hasara mbili za mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja.

### 2.1.4 Swali la 4: Mtaala


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne zinazoeleza faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimi 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 2,939 (89.8%) walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 10.2 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 62 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 27.8 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, waliopata alama 3 hadi 4 (27.8%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Mtaala*, hivyo walieleza vizuri faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja. Watahiniwa waliopata alama zote nne (4.4%) walitoa majibu yanayoendana na kilichoulizwa kwenye swali. Majibu ya watahiniwa hao yalidhihirisha kuwa, walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Mtaala*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


4

(i) Inatusaidia walimu kutokutofautiana katika Maudhui katika ufundishaji na Ujifunzaji

(ii) Inatusaidia walimu kuwa na mfanano katika ufundishaji ~~katika~~ kwa kuangalia njia na mbinu zilizopendekezwa katika mtaala huo ili kwenda sambamba katika suala zima la Ufundishaji

(iii) Inatusaidia walimu kutokutoka nje ya mada zilizopendekezwa zifundishwe katika mtaala huo.


(iv) Inatusaidia walimu katika suala zima la kuthibiti mfumo wa elimu katika ufundishaji na Ujifunzaji kupitia mtaala huo wa aina moja

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alitoa hoja nne zinazoelezea faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja kwa usahihi.

Aidha, asilimia 62 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walishindwa kutoa majibu yote kwa usahihi na baadhi yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja wapo aliandika majibu sahihi ambayo ni: *kuwa na mfanano katika ufundishaji na ujifunzaji* na *walimu kupanga maudhui ya masomo yaliyopo kwenye mtaala bila kutoka nje ya maada husika*. Hoja dhaifu zilizotolewa na mtahiniwa huyo ni: *husaidia kuleta tofauti ya elimu kati ya nchi moja na nyingine* na *husaidia mwalimu kujua mbinu na njia bora ya ufundishaji*. Mtahiniwa mwingine alitoa faida ambazo ni: *husaidia kutolewa kwa maarifa sawa kwa watu wa aina zote, husaidia katika kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji kwa urahisi katika nchi, husaidia kubaini maendeleo ya kitaaluma kwa urahisi* na *husaidia kufanya upimaji tamati wa aina moja*. Katika majibu yaliyotolewa na mtahiniwa, hoja tatu za mwisho zinafanana, hivyo kumfanya apate alama za wastani. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha.

Kwa upande mwingine, asilimia 10.2 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa wachache kati yao (0.6%) walipata sifuri kwa sababu hawakuwa na maarifa kuhusu faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja ni: *mwalimu hatoweza kutumia mbinu sahihi, mwalimu hatoweza kuandaa azimio la kazi, mwalimu hatoweza kuandaa zana sahihi za kufundishia na kujifunzia* na *mwalimu hatoweza kumshirikisha mwalimu mwingine somo lake*. Pia mtahiniwa mwingine alitaja faida kama vile: *kutolewa ajira za wataalamu watakaohusika na mtaala huo, kupandishwa mshahara kwa wataalamu mbalimbali wanaohusika na mtaala, kukua kwa miradi mbalimbali ya nchi* na *kuongezwa kwa nguvukazi katika sekta mbalimbali.* Kimsingi watahiniwa walitakiwa kueleza faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja ambazo ni: *kuwa na mfanano katika ufundishaji na ujifunzaji, utawezesha kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji inayofanana; huleta ufanisi zaidi katika ufundishaji kwa kuchagua na kupanga mbinu za ufundishaji* na *kupunguza gharama za utungaji na uchapishaji wa vitabu vya kiada.* Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



4
i/ Kutotofautiana kwa Maudhui; Kupishana kwa kila shule kusoma Masomo yako pia
ii/ Kuwepo kwa tofauti za Masomo, Mada na Madalasa kwa kuwa kila Mtaala utakuwa na Masomo yako, Mada zako na Madaloso yako yatatoja
iii/ Kutofikiwa kwa Malengo ya Mtaala; Malengo ya Mtaala hayatatimia kwa sababu ya kutofautiana kwa walengwa.
iv/ Kutokuwepo kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kwa kuwa kila mtaala utakuwa unatoa vifaa vyao.

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alieleza hasara za nchi kuwa na mtaala wa aina moja, badala ya faida za nchi kuwa na mtaala wa aina moja.

### 2.1.5 Swali la 5: Upimaji katika Elimu


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutafuta wastani, modi, mediani na mfiko wa matokeo ya wanafunzi saba: 27, 65, 56, 53, 72, 63 na 56. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 2,885 (88.2%) walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, asilimia 11.8 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 18.7 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 69.5 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 69.5 walitafuta na kupata kwa usahihi wastani, modi, mediani na mfiko wa matokeo ya wanafunzi saba. Watahiniwa waliopata alama zote nne (33.8%) walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika kipengele cha *Uchambuzi na Tafsiri ya Matokeo ya Majaribio na Mitihani*. Pia walitoa tafsiri sahihi ya dhana zilizoulizwa, hivyo kuwafanya wakokotoe na kupata majibu sahihi. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali hili.



5 a) Wastani = Jumla ya alama / Idadi

Wastani = (27+65+56+53+72+63+56) / 7 = 392 / 7

Wastani = 56

∴ Wastani ni 56.

b) Modi ni namba iliyojitokeza mara nyingi katika mtiririko wa alama.

∴ Modi ni 56.

c) Mediani ni namba iliyo katikati ya alama za juu na chini 27, 53, 56, 56, 63, 65, 72

∴ Mediani ni 56.

d) Mfiko = Alama kubwa − Alama ndogo.

= 72 − 27

= 45.

∴ Mfiko ni 45.


**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa alikokotoa wastani, modi, mediani na mfiko wa matokeo ya wanafunzi saba aliokuwa amepewa kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, asilimia 18.7 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama vile kutafuta mediani bila kupanga alama alizopewa kwa mtiririko wa kuanzia ndogo kwenda kubwa, au kuanzia kubwa kwenda ndogo. Mapungufu mengine ni kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana za *mfiko* na *modi*. Pia, kutokujumlisha kwa usahihi alama walizopewa ili kupata wastani yalikuwa ni mapungufu mengine. Mtahiniwa mmojawapo kwa mfano, alikokotoa kwa usahihi vipengele vya *modi = 56* na *mediani = 56*. Mtahiniwa huyo alikokotoa na kupata *wastani = 125.5* na *mfiko = 49*, majibu ambayo hayakuwa sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana hizo.

Aidha, asilimia 11.8 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao walikuwa na udhaifu katika ujumlishaji wa namba ili kupata wastani.

Halikadhalika, kutokuwa na uelewa wa dhana za mediani, modi na mfiko nako kulifanya wapate alama dhaifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipata kipengele cha kutafuta mfiko lakini alishindwa kupata alama kwenye vipengele vya modi, wastani na mediani. Watahiniwa waliopata sifuri (3.5%) walikuwa na udhaifu katika matendo ya namba yaani kujumlisha, kutoa na kugawanya. Walipotakiwa kufanya tendo la kujumlisha hawakujumlisha kwa usahihi, pia kushindwa kugawanya. Wengine hawakuwa na maarifa ya jinsi ya kutafuta modi, wastani, mfiko na mediani. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



5 - Matokeo ya wanafunzi saba yalikuwa kama ifuatavyo 27, 65, 56, 53, 72, 63 na 56 :
kutafuta

a) wastani = 27 + 65 + 56 + 53 + 72 + 63 + 56
= 492

b) Modi = 72 - 27
= 45

c) Mediani = 53


d) Mfiko = 72.

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa hakujumlisha kwa usahihi alama alizopewa na hakutambua tofauti iliopo kati ya modi na mfiko.

### 2.1.6 Swali la 6: Utafiti wa Kielimu


Mtahiniwa kwenye swali hili alitakiwa kuweka bayana sifa za suala zuri la utafiti kwa kutumia hoja nne. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu hafifu kwa kuwa watahiniwa 1,206 (36.9%) walipata alama 2 hadi 4, kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.




***Chati Na. 6:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 63.1 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 12.4 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 24.5 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 63.1 walipata alama 0 hadi 1.5. Kati yao, asilimia 49.5 walipata sifuri kwa vile hawakuwa na maarifa kuhusu sifa za suala zuri la utafiti. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha kuwa sifa za suala zuri la utafiti ni: *utafiti unapoteza muda, utafiti hudidimiza mawazo waliobuni katika swala la kuchunguza au kudadisi jambo, utafiti unaweza kuwa siyo wa kweli* na *utafiti huongeza chumvi katika taarifa*. Mtahiniwa mwingine alibainisha sifa hizo kuwa ni: *liwe na utangulizi, liwe na zana za kufanyia utafiti, liwe na muda maalumu wa kufikiwa* na *liwe na maswali, malengo na gharama zitakazotumika*. Vilevile, mtahiniwa mwingine alitoa sifa hizo kuwa ni: *kutembelea eneo husika kabla ya kuanza utafiti, kutengeneza ukaribu na watu wa eneo hilo unalotegemea kufanya utafiti, kuunda nukuu nzuri za kufanyia utafiti* na *kuandaa mazingira ya sehemu utakayofanyia utafiti na kuzijua changamoto za sehemu hiyo.* Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


6

Sifa za suala zuri la utafiti

i) Watafiti wawe wamebobea juu ya kile wanachoki
endea kukifanyia utafiti.

ii) Watafiti wawe na ujuzi wa kutosha juu ya
kile kitu wanachoenda kukifanyia utafiti

iii) Watafiti wawe na vifaa pamoja na mbinu za kuto
sha watakazo tumia katika kufanya utafiti


iv) Watafiti wawe na daftari za kuandikia taarifa
za utafiti

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali 6.

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alibainisha sifa za watafiti badala ya kubainisha sifa za suala zuri la utafiti jambo linalodhihirisha kuwa hakuelewa matakwa ya swali.

Baadhi ya watahiniwa (12.4%) walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa katika kundi hili waliandika majibu pungufu ya manne yaliyohitajika kwenye swali na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu sahihi ambayo ni: *liweze kufanyika* na *liwe wazi*. Aidha, alitoa majibu yasiyo sahihi kama vile: *litumie lugha fasaha* na *litoke kwenye mazingira*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha.

Aidha, asilimia 24.5 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa waliopata alama zote nne (13.5%) walibainisha kwa usahihi sifa nne za suala zuri la utafiti. Watahiniwa wengine katika kundi hili walibainisha sifa tatu kwa usahihi na wengine kurudia hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu sahihi yafuatayo: *lazima lifanyike katika mazingira halisi, liwe wazi na liwe na mchango katika masuala mengine ya kitafiti*. Aidha, alibainisha sifa nyingine ambayo siyo sahihi ambayo ni *liwe na mwonekano*. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




6 i) liwe na mchango katika masuala yaliyo kwisha tangulia.
ii) Suala ~~la~~ zuri la utafiti liwe wazi.
iii) Suala la utafiti liwe linaweza kufanyika kati-ka mazingira halisi.
iv) Suala zuri la utafiti liwe linapimika na mwelekeo

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alibainisha sifa nne za suala zuri la utafiti kwa usahihi.

### 2.1.7 Swali la 7: Tathmini katika Elimu


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne zinazoelezea hatua anazopaswa kuzifuata mwalimu wakati wa uandishi wa matokeo ya tathmini ya somo lake analofundisha. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani watahiniwa 1,638 (50.1%) walipata alama 2 hadi 4, kama inavyoonekana katika Chati Na.7.




***Chati Na. 7:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, asilimia 49.9 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 15.6 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 34.5 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, waliopata alama 0 hadi 1.5 (49.9%) walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo kupata alama za chini. Watahiniwa waliopata sifuri (11.9%) walitoa hoja zisizo sahihi. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa kuhusu *Tathmini ya Somo,* hivyo walitoa majibu tofauti na kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa hatua wanazopaswa kuzifuata ni: *ufaulu wa wanafunzi, mpangilio mzuri wa alama kwa kuanza ndogo kwenda kubwa, wastani wa alama zote za wanafunzi* na *mpangilio mzuri wa namba*. Mtahiniwa mwingine alieleza hatua hizo ni: *jina la shule, somo analofanyia tathmini, tarehe na mwaka*. Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika hatua zisizo sahihi ambazo ni: *kuandika kutoka namba kubwa kuja ndogo, kuandika wastani wa kila mwanafunzi, kuandika ufaulu wao kwa ujumla* na *kujua tofauti ya waliofaulu na waliofeli.* Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



i) Tathimini awali

ii) Tathimini endelevu

iii) Tathimini Tatuzi au gunduzi


iv) Tathimini tamati

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alibainisha aina za tathmini badala ya kutoa hoja zinazoelezea hatua wanazopaswa kuzifuata walimu wakati wa uandishi wa matokeo ya tathmini ya somo lake analofundisha.

Aidha, asilimia 15.6 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa katika kundi hili walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, walirudia hoja na wengine kutoa hoja dhaifu ambazo hazikustahili kupata alama zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu sahihi kama vile: *uzingatiaji wa lengo mahususi* na *usahihishaji wa kazi za wanafunzi*. Aidha, alitoa majibu yasiyo sahihi kama vile: *uzingatiaji wa umri wa wanafunzi* na *uelewa wa mwalimu katika matumizi ya zana*, hivyo kupata ufaulu wa wastani. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya uandishi wa matokeo ya tathmini ya somo.

Kwa upande mwingine, asilimia 34.5 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa walitoa hoja sahihi tatu hadi nne juu ya hatua anazopaswa kuzifuata mwalimu wakati wa uandishi wa matokeo ya tathmini ya somo lake analofundisha. Watahiniwa waliopata alama zote nne (22.9%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipengele cha *Utaratibu wa Kufanya Tathmini Katika Somo* hivyo walipata alama za juu katika swali hili. Hii inachangiwa na uzoefu walioupata katika mazoezi ya kufundisha kwa vitendo wakiwa mwaka wa kwanza na wa pili. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



7 i) kuchunguza malengo ya somo.
ii) kuchunguza Ushiriki na Uwezo wa wanafunzi darasani katika kufanya mazoezi, majaribio na kazi mbalimbali
iii) kupima, malengo yaliweza kufanikiwa kwa kutoa zoezi
iv) kusahihisha na kuweka alama za matokeo ili kubaini malengo yaliweza kufanikiwa na kuandika taarifa za tathmini.

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.2, mtahiniwa alitoa hoja nne zinazoelezea hatua anazopaswa kuzifuata mwalimu wakati wa uandishi wa matokeo ya tathmini ya somo analofundisha kwa usahihi.

### 2.1.8 Swali la 8: Maendeleo ya Elimu Tanzania


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi sifa nne zinazobainisha mfumo rasmi wa elimu. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 3,099 (94.7%) walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




***Chati Na. 8:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, asilimia 5.3 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5; asilimia 59.4 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 35.3 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 35.3 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walieleza kwa kifupi sifa tatu hadi nne zinazobainisha mfumo rasmi wa elimu. Watahiniwa waliopata alama zote nne (1.2%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya mfumo rasmi wa elimu. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na mtahiniwa mmojawapo ni: *kuna wataalamu maalumu walioandaliwa kufundisha, hutumia mtaala maalumu, hutoa vyeti na tuzo mwishoni mwa kila ngazi ya mafunzo* na *kuna ratiba maalumu ya kufuata*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


8 Sifa za mfumo rasmi wa elimu.

(i) Una mtaala maalumu wa kufundisha katika utoaji wa elimu.

(ii) Una walimu maalumu wa kutoa elimu.

(iii) Una utoaji wa vyeti mwishoni mwa mafunzo.

(iv) Una njia maalumu za kufanya upimaji na tathmini katika elimu.


**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alieleza kwa kifupi sifa nne zinazobainisha mfumo rasmi wa elimu kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, asilimia 59.4 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama vile; kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kurudia hoja na kutoa hoja pungufu au kutoa hoja dhaifu zisizostahili kupata alama zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu sahihi kama vile: *hufuata mtaala rasmi* na *vyeti hutolewa baada ya mwanafunzi kuhitimu kila ngazi ya mafunzo*. Pia, alitoa majibu yasiyo sahihi kama vile: *mafunzo yanayotolewa yamejikita zaidi kwenye nadharia kuliko vitendo* na *una maandhari ya*

*kujifunzia*. Mtahiniwa mwingine alibaini sifa hizo kuwa: *unakuwa chini ya usimamizi, unakuwa na mazingira maalum, unakuwa na wataalamu* na *unagawa vyeti*. Mtahiniwa alitoa majibu ambayo hayakuwa yamejitosheleza hivyo kupata alama za wastani. Majibu haya yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya sifa zinazobainisha mfumo rasmi wa elimu.

Aidha, asilimia 5.3 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana ya *mfumo rasmi wa elimu*. Watahiniwa hao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitoa hoja dhaifu. Watahiniwa wachache (0.5%) walipata sifuri kwa sababu hawakuwa na maarifa katika kipengele cha dhana ya elimu, hususani mfumo rasmi wa elimu, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza sifa zinazobainisha mfumo rasmi wa elimu ni: *kujiamini, ushirikiano mzuri, maendeleo* na *falsafa ya nchi*. Mtahiniwa mwingine alieleza sifa hizo kuwa ni: *kuwa na uongozi bora wa ngazi ya elimu na ubora wa viongozi hao, ufaulu wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu, kuzingatia mfumo mzuri wa siasa* na *kuzingatia usalama wa hali ya hewa (magonjwa).* Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



8
Sifa za mfumo
- Kuwepo kwa demokrasia
- Kuwepo kwa ~~usah~~ usawa wa binadamu
- Kuwepo kwa mgawanyo wa madaraka
- Kuchagua na kuchaguliwa

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa aliandika hoja zinazohusu mambo ya demokrasia badala ya sifa zinazobainisha mfumo rasmi wa elimu.

### 2.1.9 Swali la 9: Elimu ya Watu Wazima


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi madhumuni ya elimu ya watu wazima kama yalivyoelezwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1970 kwa kutumia hoja nne. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 2,447 (74.8%) walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 9.




***Chati Na. 9****: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa, asilimia 25.2 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 63.2 alama 2 hadi 2.5 na asilimia 11.6 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 25.3 walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa katika kundi hili walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, au walitoa hoja pungufu. Watahiniwa wengine walitoa hoja zenye kujirudia au kutoa hoja ambazo ni dhaifu hivyo kupata alama pungufu. Watahiniwa waliopata sifuri (2.2%) hawakuwa na maarifa kuhusu madhumuni ya elimu ya watu wazima kama yalivyoelezwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1970. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza madhumuni hayo kuwa ni: *kuleta usawa wa kijinsia, usawa katika demokrasia* na *ujamaa na kujitegemea*. Mtahiniwa mwingine alieleza madhumuni hayo kuwa ni: *kuzingatia haki na usawa, kuzingatia kazi kwa kila mtu, kuzingatia utu na kuzingatia demokrasia*. Aidha, mtahiniwa mwingine alieleza kuwa madhumini hayo ni: *kurekebisha zana na vifaa vya ufundishaji, kufundisha kwa nadharia kwenda vitendo, kuendeleza kisomo chenye manufaa* na *mfumo wa elimu kuwa na mtaala wa aina moja*. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


9 i) kuanzishwa kwa chama cha Elimu ya watu wazima nchini Tanzania CHEWATA
ii) kuanzishwa kwa kampeni ya elimu ya watu wazima mtu ni afya
iii) kuanzishwa kwa idara ya elimu ya wafanya kaei
iv) kuanzishwa kwa idara ya elimu ya watu wazima


**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa alieleza baadhi ya mikakati ya kuimarisha elimu ya watu wazima nchini, badala ya kueleza madhumuni ya elimu ya watu wazima kama yalivyoelezwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1970.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 63.2 walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa katika kundi hili walieleza hoja ambazo ni dhaifu na wengine kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, hivyo walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza madhumuni ya elimu ya watu wazimia kuwa ni: *kupunguza idadi kubwa ya watu wasiojua kusoma na kuandika* na *kuwasaidia katika shughuli zao mbalimbali za ujasiriamali*. Aidha alitoa hoja ambazo ni marudio ya hoja nyingine kama vile: *kusaidia kupunguza ujinga* na *kuandaa watu wanaojua kusoma na kuandika*. Mtahiniwa mwingine katika kundi hili alieleza malengo hayo kuwa ni: *kuondoa ujinga, kujenga jamii iliyoelimika, kupunguza utegemezi wa kuajiriwa* na *watu wajiajiri wenyewe kwa kufanya kazi zenye manufaa*. Katika majibu ya mtahiniwa huyo, hoja ya kwanza na ya pili zina mfanano. Pia hoja ya tatu na ya nne zina mfanano, hivyo kumfanya apate alama za wastani. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya madhumuni ya elimu ya watu wazima kama yalivyoelezwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1970.

Kwa upande mwingine, asilimia 11.6 ya watahiniwa walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa walieleza kwa kifupi madhumuni matatu hadi manne ya elimu ya watu wazima. Watahiniwa waliopata alama zote nne (2.2%) walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Dhana ya Elimu ya Watu Wazima*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa madhumuni ya elimu ya watu wazimia ni: *kujikwamua katoka hali duni ya kimaisha*, *kumsaidia mtu namna*

*ya kuzalisha mali, kumsaidia mtu njia za kutunza mazingira* na *kuwawezesha watu kushiriki vema shughuli za kisiasa*. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeelewa matakwa ya swali na alikuwa na maarifa ya kutosha.



9
Yafuatayo ni madhumuni ya elimu ya watu wazima Kama yalivyoelezwa na mwalimu Nyerere mwaka 1970.
i) Kuwezesha Kupata mbinu bora za Kutunza afya na mazingira. Elimu ilitolewa ili wanafunzi watu wazima waweze Kutunza afya na mazingira.
ii) Kuwezesha Kupata mbinu bora za uzalishaji mali. mfano Katika Kilimo.
iii) Kuwezesha Kupata elimu Kama iliyotolewa Shule za msingi, Sekondari na vyuoni ili aweze Kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu pamoja na Stadi nyingine za maisha mfano ufundi.
iv) Kumwezesha mwanafunzi mtu mzima Kujikomboa Kifikra na Kushiriki Katika shughuli za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni.

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alieleza kwa kifupi na kwa usahihi madhumuni manne ya elimu ya watu wazima kama yalivyoelezwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1970.

### 2.1.10 Swali la 10: Uongozi wa Elimu Tanzania


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne zinazoelezea viashiria vya uongozi bora wa shule. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 2,701 (82.5%) walipata alama 2 hadi 4. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa, asilimia 17.5 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5, asilimia 19.6% alama 2 hadi 2.5 na asilimia 62.9 alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 62.9 walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Uongozi wa Elimu Tanzania*. Vilevile, walitoa hoja tatu hadi nne zilizoelezea viashiria vya uongozi bora wa shule. Watahiniwa waliopata alama zote nne (33.3%) walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sifa za uongozi bora wa shule, hivyo kutoa hoja nne ambazo zilikuwa sahihi. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


10

i) Wanafunzi kufaulu vizuri masomo yao

ii) wanafunzi na walimu kuwa na nidhamu nzuri

iii) Miundombinu mizuri ya Mazingira ya shule mfano Majengo, viunga vya maua kuwa vizuri kutokana na uongozi bora

iv) ukweli, uwazi na kujituma kwa walimu na viongozi wote wa shule hiyo.


**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.1, mtahiniwa alieleza kwa kifupi viashiria vinne vya uongozi bora wa shule kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, asilimia 19.6 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 2.5. Watahiniwa hao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine kutoa hoja dhaifu hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja nne ambazo zilikuwa ni dhaifu, hivyo kufanya apate alama za wastani. Alieleza viashiria vya uongozi bora shuleni ambavyo ni dhaifu kama vile: *ufaulu wa wanafunzi, nidhamu ya wanafunzi, mahudhurio ya wanafunzi* na *utunzaji wa mazingira ya shule*. Hoja hizi zingekuwa sahihi endapo mtahiniwa angeeleza ni kwa kiwango gani hoja hizo zinajidhihirisha. Kwa mfano, *ufaulu mzuri wa wanafunzi* au *nidhamu bora ya wanafunzi*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya viashiria vya uongozi bora wa shule.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, asilimia 17.5 walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya uongozi bora wa shule, hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa waliopata sifuri (5.8%) walitoa majibu yote yasiyo sahihi kutokana na kutokuwa na maarifa kuhusu dhana ya uongozi bora wa shule. Kwa mfano, mmoja wa watahiniwa alitoa viashiria kama vile: *kuangalia haiba ya viongozi*, *kuwepo na mpangilio mzuri*, *kuwepo na kiongozi mwenye nidhamu* na *kuangalia matendo yao*. Mtahiniwa mwingine alitoa viashiria ambavyo ni: *kujiamini*,

*ujasiri, utii* na *usafi*. Majibu haya ya watahiniwa hayakuwa sahihi kwani walitakiwa kutoa hoja zinazoelezea viashiria vya uongozi bora wa shule kama vile: *wanafunzi kuwa na ujuzi wa kudumu katika kusoma, kuandika na Kuhesabu, kupanda kwa alama za ufaulu wa wanafunzi katika mitihani, kuongezeka kwa uwezo wa wahitimu wa kuweza kujitegemea, wanafunzi kupenda kufanya kazi kwa kujituma* na *wanafunzi kuwa na maadili mema*. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


10

→ Awe anakubali kukosolewa anapokosea

→ Awe mpole

→ Awe anaweza kutunza siri.

→ Awe msafi muda wote.

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.


Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alitoa hoja zinazoelezea haiba ya kiongozi badala ya kueleza kwa kifupi viashiria vinne vya uongozi bora wa shule.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Maswali katika sehemu B yalitoka katika mada nne (4) ambazo ni*: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto, Ufundishaji, Upimaji Katika Elimu* na *Elimu ya Watu Wazima*. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15), hivyo kufanya jumla ya alama sitini (60).

### 2.2.1 Swali la 11: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza mambo sita yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 3,143 (96.1%) walipata alama 6 hadi 14.5. Chati Na.11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




***Chati Na. 11:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, asilimia 3.9 ya watahiniwa walipata alama 0.5 hadi 5.5, asilimia 75.6 alama 6 hadi 10 na asilimia 20.5 alama 10.5 hadi 15. Aidha, hakuna mtahiniwa aliyepata alama sifuri katika swali hili hivyo ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 0.5 hadi 14.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, waliopata alama 10.5 hadi 14.5 (20.5%) walieleza mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa kwa usahihi. Kati yao, waliopata alama 14 hadi 14.5 (0.4%) walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa. Wengi kati yao walianza na utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

Yafuatayo ni mambo yanayoathiri ukuaji wa mtoto mara baada ya kuzaliwa:-


Lishe duni; jambo la kwanza linalopelekea kwa kiasi kikubwa kuathirika kwa maendeleo ya ukuaji wa mwanafunzi au mtoto. ni kutokana cha kutopata lishe bora. ambapo inapelekea mwili wa mtoto kuwa dhaifu na kuathiri ukuaji wake.

Magonjwa; suala lingine linaloathiri pia ukuaji wa maendeleo ya watoto ni kutokana na watoto kuathiriwa na magonjwa mbalimbali. pindi pale anapokuwa amezaliwa. Magonjwa hayo yanaweza kuwa ya kurithi au yasiwe ya kurithi.

Malezi mabaya ya walezi; pia masuala ya malezi ya watoto pia yanaweza kupelekea kuathiri afya ya ukuaji wa mtoto. baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa na malezi mabaya ambayo yamekuwa yakiathiri sana ukuaji wa watoto kiafya na kitabia.

Umaskini; katika suala la umaskini hili limechangia kwa kiasi kikubwa pia kuathiri masuala mazima ya ukuaji wa wanafunzi aidha iwe. Kutokana na hali ngumu ya maisha. wazazi wanashindwa kupata mahitaji muhimu kama chakula, mavazi na malazi kwa ajili ya kutunza famili lia zao.

Utandawazi; hili limekuwa moja ya janga kubwa sana katika nchi mbalimbali. Kwa hivi sasa ukuaji wa watoto wengi mara baada ya



11 Cont. Kuzaliwa wazazi wengi wamekuwa wakiwalea watoto wao katika mitindo ya kisasa ya maisha wanayoyaona mitandaoni. Mfano baadhi ya wazazi mara baada ya kuzaa huwa hawawanyonyeshi watoto wao kwa kusema kwamba maziwa yao yatawahi kulala au kusinyaa. hivyo huathiri afya za watoto kwa kuwalisha maziwa ya makopo.

Migogoro ya kifamilia; pia suala la kutokea kwa migogoro mbalimbali katika familia kumepelekea baadhi ya watoto kuathiriwa kiakili na kiafya. kutokana na hali ya kuwa na changamoto mbalimbali za migogoro ya familia, hivyo kupelekea kuathiri ukuaji wa mtoto kitabia, kimaono na hata kimwili.

Hivyobasi; hayo ndiyo baadhi ya mambo ambayo yanapelekea ukuaji wa watoto wengi kuathiriwa kiakili, kitabia, kimaono na hata kimwili mara tu baada ya kuzaliwa hii ni kutokana na kuwa na hali ya matatizo ya kifamilia. Hivyo wazazi na walezi wajitahidi kudhibiti hili ili kujenga ukuaji mzuri wa watoto baada ya kuzaliwa.

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.1 mtahiniwa alibaini kwa usahihi mambo sita yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa, japo baadhi ya mambo hayo hakuyatolea maelezo ya kutosheleza.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, waliopata alama 6 hadi 10 (75.6%) walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa. Watahiniwa hao walibaini mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa, ingawa walionesha kuwa na mapungufu mbalimbali katika insha zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *lishe duni*, *mazingira ya shule*, *magonjwa*, *ukuaji kimwili*, *mazingira ya kifamilia* na *uruthi.* Hoja zote zinakubalika isipokuwa hoja ya *ukuaji kimwili* ambayo ni dhaifu sana. Hata hivyo, mtahiniwa hakutoa maelezo ya kina namna hoja hizo zinavyoathiri ukuaji wa mtoto. Pia, mtahiniwa mwingine alibaini sababu ambazo ni: *lishe duni, uwezo wa kiuchumi, magonjwa mbalimbali, hali ya hewa, mazingira*

*duni na maendeleo ya sayansi na teknolojia*. Hoja zote alizotoa mtahiniwa zilikuwa sahihi, isipokuwa hoja ya *uwezo wa kiuchumi* ni marudio ya hoja ya *lishe duni*. Aidha, hoja za *hali ya hewa* na *mazingira duni* hakuzitolea maelezo yanayostahili, hivyo kumfanya apate alama za wastani. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha.


Kwa upande mwingine, asilimia 3.9 ya watahiniwa walipata alama 0.5 hadi 5.5. Watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa. Hivyo, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine kushindwa kuelezea hoja ambazo zilikuwa ni sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea kuwa mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa ni: *unene, tabia mbaya au nzuri, rangi (weupe au weusi), upole, urefu na ukarimu*. Mtahiniwa mwingine kati ya hao alichanganya mambo sahihi na yasiyo sahihi yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa kama ifuatavyo: *mtoto kutokupewa lishe/chakula bora, mtoto kutokupewa chanjo za magonjwa ya kuambukiza, mtoto kutokupewa matibabu ya msingi au sahihi, mtoto kutokupewa vitu mbalimbali vya kuchezea, mtoto kutokupewa ulinzi na ushirikiano kutoka kwa wazazi* na *matumizi ya pombe, sigara na madawa ya kulevya kwa mama*. Mtahiniwa mwingine alieleza mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa kuwa ni: *mazingira, malezi, kukua kimwili, kukua kiakili, kukua kihaiba na urithi.* Watahiniwa walitakiwa kutoa majibu sahihi ambavyo ni: *malezi, hali ya kiuchumi ya jamii, mila na desturi za jamii, hali ya hewa, maradhi* na *maendeleo ya sayansi na teknolojia*. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali katika swali hili.

11 Ukuaji wa Mtoto ni hali ya mtoto kubadilika au kuongezeka umbo la mwili kulingana na akili aliyonayo pia kuongezeka kufikili. Yafuatayo ni mambo ambayo yanaonyesha ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa, kama ifuatavyo.

Kiakili, ukuaji wa mtoto hutegemea kulingana na akili yake na umri anaokuwa nao hii vyo mtoto mwenye umri wa miaka miwili si sawa na mtoto mwenye umri wa miaka mitano mapopelekea akili za watoto hao zik alingana au mtoto mwenye miaka mitano ku wa sawa na mtoto mwenye miaka miwili hapo ukuaji wa mtoto hauendelei.

Kimwili, ukuaji wa mtoto kimwili ni kuongezeka kwa baadhi ya Viungo vya mwi li hapa ndipo tunaona mtoto anakuwa anapo ongezeka urefu, unene, kwani mtoto mwenye umri wa miaka mitano si sawa na mtoto mwe nye umri wa miaka nane au tisi hivyo muo nekano wao wa kimwili unakuwa tofauti

Kihaiba, ukuaji wa mtoto unaweza kuonekana ata haiba yake aliyo nayo kwa ni pale anapokuwa anaonesha haiba yake aliyonayo mtoto, huyo anaweza akawa na haiba inayoendana na umri wake mfano mtoto mwenye umri wa miaka mitatu si sawa na mtoto mwenye miaka kumi, mtoto mwe nye umri wa miaka mitatu, hajifeadi na anakuwa mara nyingi anahudumiwa na mlezi au mzazi lakini muonekano wa mtoto mwe nye umri wa miaka kumi anaweza wa kuji




Cont. udumua, Mtoto mwenye umri wa miaka kumi
hata mawazi yake anayapenda na hutaka kuoneka
na msafi muda wote.
Kimaono, maono yanaweza kutoonyesha ku
wa mwanafunzi au mtoto huyo anakuwa kwa
ni anakuwa na uwezo wa kudadisi au
kuuliza maswali pale anapoona kuwa ajelle
wa na kuweza kutafuta ufumbuzi kuhu
su jambo amlalo anataka kulijua anaweza
kudadisi mambo magumu. Uwezo wa kufi
kili unaongezeka.
Kitabia, mtoto ukuaji wake unaonekana
ata kulingana na tabia kwani mtoto mwenye
umri wa miaka miwili anakuwa na tabia
ya kumtegemea mzazi wake yaani mama yake
katika kumuudumia kwa kila kitu na hata
pia kujisaidia kuvenye nguo lakini mtoto
mwenye umri wa miaka mitano ataongea
pale anapotaka kujisaidia na kuweza
kwenda kujisaidia maeneo husika.
Kijamii mtoto tunamuangalia amekuaje
au ukuaji wake unaendana na umri wak
e kwani anatakiwa ajitegemee yeye
mwenyewe katika jamii inayomzunguka na ku
angalia anatenda kama jamii inavyo taka
hivyo hapa hujifunza michezo, kutumia lugh
a mama na kufanya shughuli ndogondo
go kama kuosha vyombo hii kuweza kuje
nga stadi ya kufanya kazi.

**Kielelezo Na. 11.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa alieleza nyanja mbalimbali za makuzi ya mtoto, badala ya kueleza mambo yanayoweza kuathiri ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa.

### 2.2.2 Swali la 12: Ufundishaji

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua kwa kina faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 3,242 (99.1%) walipata alama 6 hadi 14.5, kama inavyoonekana katika Chati Na. 12.




***Chati Na. 12:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa, watahiniwa wachache (0.9%) walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 34.8 alama 6 hadi 10 na asilimia 64.3% alama 10.5 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, waliopata alama 10.5 hadi 14.5 (64.3%) walikuwa na uelewa mzuri kuhusu faida na hasara za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliopata alama 14 na 14.5 (0.5%) walichambua vizuri faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

12 Mbinu ya kazi mradi ni mbinu ya ufundishaji na ujifunzaji ambayo inamtaka mwanafunzi ajifunze zaidi kwa vitendo ambapo mwalimu wa somo husika hutakiwa kuzingatia mambo mbalimbali ili kukamilisha Ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi kwa kutumia mbinu ya kazi mradi mambo hayo ni kama kuandaa mada mbalimbali na kuwapa katika makundi ili waweze kuifanyia kazi au kwa mtu mmoja mmoja. Mbinu ya kazi mradi ina faida na hasara.

Zifuatazo ni faida za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa Ufundishaji na ujifunzaji.

Humuwezesha mwanafunzi kujifunza kwa vitendo zaidi; kwasababu mbinu ya kazi mradi inaambatana zaidi na vitendo na si nadharia, kupitia hivyo humuwezesha mwanafunzi kujifunza kwa vitendo zaidi na hatimaye kumfanya aweze kuwa na maarifa ya kutosha juu ya kile alichojifunza na kuweza kuhusianisha mada alizojifunza na kwa vitendo zaidi, hivyo kazi mradi inafaa katika kufundishia.

Humjengea mwanafunzi kumbukumbu ya muda mrefu, hii ni kwasababu mwanafunzi ndiye anakazi ya kutafuta maarifa na ujuzi mbalimbali atakaoutumia kutafuta majibu na suluhisho ya kazi zilizotolewa na mwalimu kwa njia ya kazi mradi. Kwamfano mwanafunzi akichagua mada ya "Ajali za barabarani" hana budi kwenda katika vituo mbalimbali vinavyohusiana na mambo ya barabarani ili aweze kujifunza kwa Undani zaidi.

ont. Humsaidia mwanafunzi kuhusianisha mada za darasani na mazingira halisi, kwasababu kwa vyovyote vile kazi mradi hutakiwa kufanywa nje ya darasa na hata nje ya wilaya, kijiji au mkoa mfano wanafunzi huweza kuchagua mada za magonjwa na kwenda kufanyia hospitali kwa ajili ya kujifunza zaidi. Kwa kufanya hivyo inampelekea mwanafunzi kuhusianisha mada ambazo anafundishwa darasani na mazingira halisi.

Zifuatazo ni hasara za mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa Ufundishaji na ujifunzaji;

Hupoteza muda mwingi; wakati wa kufundisha na kujifunza kwa kutumia mbinu ya kazi mradi muda mwingi huweza kutumika kwasababu mwanafunzi anapewa mada ambayo anatakiwa kutoka nje ya shule au nje ya wilaya kwaajili ya kujifunza, mwanafunzi hutumia muda mwingi kusafiri na kupata majibu endapo atakwenda kufanyia kazi mradi nje ya kituo chake cha kujifunzia.

Hutumia gharama ili iweze kukamilika, kwasababu baada ya kuandika mambo yote ambayo yamefanyika kazi kwa njia ya kazi mradi mwanafunzi anatakiwa kuchapisha kazi zake kwa mashine, kupiga picha ya vitu mbalimbali na hata kutoa kopi za nakala mbalimbali, mambo yote ambayo yanafanyika huhitaji kiasi cha fedha ili kukamilisha kazi hivyo mwanafunzi hutakiwa kuingia gharama ili kukamilisha nakala hizo.

Cont.

Baadhi ya wanafunzi huweza kushiriki kwa kiasi kidogo, kwasababu mwanafunzi ndiye mtendaji mkuu, katika kundi huwepo viongozi ambao ni wanafunzi na si walimu hivyo inakuwa ni ngumu wao kwa wao kujiongoza na kuweza kushiriki vema katika kujifunza kwa mbinu ya kazi mradi. Wanafunzi kutoshiriki ipasavyo hutokea hasa pale wanapo-kuwa katika makundi ya kujifunza kwa kazi mradi na si kwa mtu mmoja mmoja.

Hivyobasi, mbinu ya kazi mradi inafaa kutumika katika mchakato wa kufundishia na kujifunzia lakini walimu hatuna budi kuwa karibu na wanafunzi bega kwa bega ili kuweza kukamilisha mchakato huo na kuweza kupunguza au kutatua changamoto ambazo zingewakumba wakati wa kujifunza kwa mbinu ya kazi mradi.

**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12.


Katika Kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa alichambua vizuri faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa upande mwingine, asilimia 34.8 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 10. Watahiniwa hao walishindwa kutoa maelezo sahihi katika hoja zao. Miongoni mwa watahiniwa hao wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine kutoa hoja ambazo ni dhaifu hivyo kupata alama pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa faida za mbinu ya kazi mradi ni: *inamrahisisishia mwalimu ufundishaji wake*, *inasaidia kukuza ushirikiano miongoni mwa wanafunzi* na *inasaidia wanafunzi kuelewa vizuri somo*. Vilevile, aliandika hasara za mbinu ya kazi mradi kuwa ni: *inasababisha wanafunzi wengine kutegea katika ujifunzaji*, *inaibua uoga na wanafunzi kutokulipenda somo* na *siyo njia shirikishi kati ya mwalimu na mwanafunzi*. Mtahiniwa mwingine aliandika faida ambazo ni: *inatunza kumbukumbu ya kudumu*, *inaleta umakini* na *inafikilisha*. Pia, alibaini hasara kama vile:

*inachukua muda mrefu* na *inaleta kelele isiposimamiwa vizuri*. Hoja zote zinauhalisia, lakini mtahiniwa hakutoa maelezo ya kutosheleza hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache (0.9%) waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na uelewa mdogo kuhusu faida na hasara za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, hivyo kutoa hoja zenye usahihi kidogo. Watahiniwa waliopata alama za chini (5.5%) hawakuwa na maarifa kuhusu mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, hivyo walitoa majibu tofauti na ilivyoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua faida zifuatazo: *humsaidia mwalimu kufundisha vitu vichache, huokoa muda katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji* na *husaidia kupata maarifa mengi zaidi*. Alichambua pia hasara ambazo ni: *huchosha wakati wa tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu hushiriki kiasi kidogo sana kwa kuwaelekeza wanafunzi na humfanya mwanafunzi kutokuwa na ari ya kujifunza.*

Vilevile, mtahiniwa mwingine alichambua faida kama vile: *husaidia mwalimu kujua maendeleo ya mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, humsaidia mwalimu kutambua kiqsi cha uelewa wa mwanafunzi* na *humsaidia mwalimu kugundua changamoto mbalimbali ambazo anakumbana nazo kwenye ujifunzaji*. Alichambua pia hasara kama vile: *haimfikirishi mwanafunzi, haimjengei mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu* na *haimjengei mwanafunzi udadisi.* Badala yake, watahiniwa walitakiwa kuchambua faida za mbinu ya kazi mradi kama vile: *hushirikisha milango mingi ya fahamu, huchochea udadisi katika ujifunzaji na ufundishaji, hukuza uwezo wa kufikiri kwa mwanafunzi, hujenga ushirikiano baina ya wanafunzi* na *hukuza stadi za kusikiliza na kuandika.* Pia, walitakiwa kuchambua hasara kama vile: *hutumia gharama katika ufundishaji na ujifunzaji*, *huhitaji muda mrefu katika ufundishaji na ujifunzaji* na *huweza kuchochea udanganyifu isiposimamiwa vizuri*. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 12 kwa usahihi.


12

Mbinu ya kazi mradi, ni aina ya mbinu an ayotumia mwalimu darasani kwa lengo la kura hisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa mwana funzi. Kuna mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo ni: Mbinu ya majadiliano, mbinu ya maswali na majibu, matembezi Garali, na Kadha lika. Zifuatazo ni faida za kutumia mbinu hii ya kazi ya mradi:

Hurahisisha ufundishaji kwa mwalimu. Mbinu hii inapotumiwa katika ufundishaji huweza kumpa mwalimu ile Ali ya kufundi sha, kwa kutoa maanifa kwa wanafunzi w ake. Darasani pia wanafunzi kuweza kuelewa.

Hutumia muda mfupi katika ufundishaji wake, Pindi mwalimu anapotumia mbinu mbali mbali za ufundishaji, ak zana humsaidia mwalimu kuokoa muda, kat kuliko kufundi sha kwa Nadharia bila ya hata vitendo.

Humsaidia mwalimu kufundisha kwa mpangilio mzuri wa maudhui. Kutokana na hii mbinu ambayo ambitumia katika suala nzima la ufundishaji. Zifuatazo ni hasara ya mbinu hii katika ufundishaji na ujifunzaji.

Ni ngumu mwanafunzi kuelewa vizuri mbinu hii sio rahisi kwa mwanafunzi akiwa darasani, Inampa ugumu mwanafunzi, anael ewa kwa kasi ndogo sana.

Haimpi mwanafunzi uwezo wa kufikiri kwa sababu ni ngumu katika ufundishaji wake hiyo kusababisha mwanafunzi huyo kutolipe nda somo, na kutopata maanifa ya kutosha

Cont.

Haimpi Ali ya kujifunza, Mbinu hii inampa nya mwanafunzi kutokua na utayari na kupoke a maanifa yanayofundishwa.


Kwa ujumla, Walimu wanapaswa kutumia mbinu ambazo ni rahisi katika ufundishaji pia uji funzaji wao darasani.

**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na.12.2, mtahiniwa alichambua mbinu ya kazi mradi kama zana kwa mwalimu. Aidha, alishindwa kutofautisha kati ya faida na hasara za mbinu ya kazi mradi.

### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza mambo sita anayopaswa kuyazingatia katika kutekeleza jukumu la kutunga maswali ya "Kweli au Si kweli." Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa watahiniwa 2,227 (68.1%) walipata alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.




***Chati Na. 13:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa, asilimia 31.9 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5.5, asilimia 60.8 alama 6 hadi 10 na asilimia 7.3 alama 10.5 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, waliopata alama 0 hadi 5.5 (31.9%) hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utungaji wa maswali ya "Kweli au Si kweli", hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa waliopata sifuri (0.9%) walitoa hoja dhaifu zisizoendana na matakwa ya swali, hivyo walitoka nje ya kilichoulizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa mambo ya kuzingatiwa wakati wa utungaji wa maswali ya "Kweli au Si kweli" ni: *kuchagua mada utakazotumia katika kutunga maswali, kujua idadi ya maswali, kujua muda*

*yatakayofanyika maswali, kutunga maswali kulingana na uwezo na uelewa wa wanafunzi, kujua alama kwa kila swali* na *kuandaa matokeo.* Mtahiniwa mwingine alieleza kuwa mambo ya kuzingatiwa ni: *jina la mtihani, somo, darasa, muhula, sehemu za mtihani* na *jumla ya alama zote zilizopo kwenye mtihani mzima.* Aidha, mtahiniwa mwingine alieleza kuwa mambo anayopaswa kuyazingatia ni: *aina ya swali, upimikaji wa swali, muda, majibu ya maswali, alama za swali* na *jumla ya maksi zote*. Majibu ya watahiniwa hao yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utunzi wa maswali ya "Kweli au Si kweli". Wengine hawakuelewa matakwa ya swali kama inavyoonekana katika sampuli ya majibu ya mmoja wa watahiniwa katika Kielelezo 13.1.

nt.

Kutunga maswali ni kitendo cha kuchambua, kuchanganua, na kufafanua maswali mbali mbali yanayo weza kufaa kwa ajili ya kuweza kujua ni kwa namna gani mwanafunzi ameweza kuelewa kile alichofundishwa kwa kujibu maswali hayo.


Yafuatayo ni mambo yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kutunga maswali ya kweli au si kweli.

Maarifa, mwalimu anapo tunga swali la kweli au sikweli anapaswa kuhakikisha kwamba swali hili lina zingatia kujenga maarifa au kupima maarifa aliyo kuwa nayo mwanafunzi au la kama halipimi maarifa halitakuwi kutumika katika upimaji.

Ufahamu, pia maswali ya kweli au si kweli yanapaswa kuwa yanapima ufahamu wa mwanafunzi, yaani ni kwa namna gani mwanafunzi anaelewa jambo husika, kwa maana hiyo mwalimu anapotunga swali la kweli au si kweli anapaswa kuhakikisha kwamba swali alilolitunga linalenga kupima ufahamu.

Utambuzi, maswali ya kweli au si kweli pia yanalenga kupima utambuzi wa mwanafunzi, yaani ni kwa namna gani mwanafunzi anatambua mambo mbali mbali hivyo mwalimu anapotunga maswali hayo anapaswa kuzingatia hilo pia.

Stadi, pia mwalimu anapo tunga maswali ya kweli au si kweli anapaswa kuhakikisha kwamba swali analolitunga lina lenga kupima ujuzi binafsi


wa mwanafunzi alio kawa nao katika ufaha
mu wake na ujibuji wa maswali kwa ujumla
Uchanganuzi, mwalimu anapo andika au kutunga
swali la kweli au si kweli anapaswa kuba
kikisha au kuzingatia kwamba swali ali
lolioandika amekweza kuchanganua na kulipo
fursa ili liweze kutumika kama swali la kwe
li au si kweli.
Tathimini. pia swali la kweli au si kweli ka
bla ya kulitumia au kulitoa kwenye mitiha
ni au jaribio linapaswa kufanyiwa tathi
mini kwanza ili kuweza kutambua kiwa
ngo cha swali.
Hivyo basi mwalimu anapotunga maswali ya k
weli au si kweli anapaswa kuhakikisha kwam
ba inazingatia mambo yote ya muhimu ili
kuweza kupata maswali yanayo weza ku
mpima mwanafunzi uwezo wake wa kufi
kiri na kadhalika.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.

Katika Kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa alieleza kuhusu ngazi za utambuzi, badala ya kueleza mambo anayopaswa kuyazingatia katika kutekeleza jukumu la kutunga maswali ya “Kweli au Si kweli.”

Kwa upande mwingine, asilimia 60.8 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 10. Watahiniwa katika kundi hili walikuwa na ufaulu wa wastani katika swali hili kwa sababu baadhi yao walitoa utangulizi sahihi, lakini walishindwa kuchambua vizuri hoja zao; na wengine walitoa hoja ambazo hazikuwa sahihi hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu sahihi ambayo ni: *kuepuka matumizi ya maneno ya moja kwa moja au ya jumla* na *kuepuka kutumia maneno yenye utata.* Hoja sahihi nyingine ilikuwa ni *kutumia lugha rahisi na inayoeleweka,* japo hoja hii ilikuwa ni marudio. Pia, mtahiniwa huyo alijumuisha hoja dhaifu ambazo ni*: kama utatumia sentensi mbili katika swali lako basi urefu wa hizo sentensi zilingane au zisipishane sana, kuepuka maelezo marefu katika swali* na *kuepuka maneno ya ukanushi*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa

hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mambo ya kuzingatia katika kutunga maswali ya “Kweli au Si kweli.”

Aidha, uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, asilimia 7.3 walipata alama 10.5 hadi 13. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utungaji wa maswali ya “Kweli au Si kweli”, walieleza mambo sita yakuzingatia katika kutunga maswali ya hayo vizuri. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata ufaulu mzuri katika swali hili.

13

Maswali ya kweli au si kweli ni Maswali ambayo hutolewa kwa Mwanafunzi ili aweze kubaini sentensi kama ni ya kweli aandike kweli au Sio ya kweli, aandike si kweli. Yapo Mambo ya kuzingatia katika utunzi wa Maswali haya kama ifuatavyo:

Epuka Sentensi za jumla. Katika utunzi wa Maswali ya kweli au si kweli Mwalimu lazima aweze kuepuka Sentensi za jumla kwa kuweza kuwafanya wanafunzi wajaribu kufikiri na kupata majibu yaliyo Sahihi.

Swali lipime kitu muhimu, Mwalimu lazima Swali lake analolitunga liweze kupima kitu muhimu ambacho amekifundisha darasani na kinachotokana na Malengo mahsusi ya Somo. Ili aweze kujua ufahamu wa wanafunzi wake.

Usitumie Misamiati Migumu katika utunzi wa Maswali yako, kwani Endapo Mwalimu atauliza Swali kwa kutumia misamiati migumu wanafunzi watashindwa kuelewa Swali linahitaji kitu gani. Hivyo Misamiati sharti iweze kueleweka kwa wanafunzi.

Cont.

Epuka Sentensi ndefu na Zenye utata, pia katika utungaji wa Maswali ya kweli au si kweli Mwalimu sharti aweze kutunga swali ambalo litakuwa rahisi kueleweka kwa wanafunzi wake. Na si kutunga sentensi ndefu ambazo zitamchanganya Mwanafunzi.

Semi Zinazozungumzia kinyume cha Maneno ziepuke daima, Mwalimu katika utunzi wa Maswali ya kweli au si kweli asitumie semi ambazo zinazungumzia kinyume cha Maneno daima. Swali liwe wazi na lisiwe na mambo mengi ambayo hayaitajika katika mtihani.

Epuka Sentensi zenye vidokezo viwili, katika kuhakikisha kuwa Mwalimu anatunga mtihani utakaoeleweka kwa wanafunzi wake lazima aepuke vidokezo ambavyo havihitajiki katika kupima yale ambayo yamekusudiwa kupimwa.


Hivyo basi, katika utunzi wa Maswali ya kweli au si kweli Mwalimu anapaswa kuzingatia Misingi yote ya utunzi wa Maswali Ili aweze kupima yale yanayotakiwa kupimwa katika mtihani wake au jaribio lake.

**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13.

Katika Kielelezo Na.13.2, mtahiniwa alieleza vizuri mambo sita anayopaswa kuyazingatia katika kutunga maswali ya “Kweli au Si kweli.”

### 2.2.4 Swali la 14: Elimu ya Watu Wazima

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua wadau sita wa elimu ya watu wazima waliotoa mchango wao katika kuendeleza elimu hiyo hapa Tanzania kwa kutumia mifano halisi. Jumla ya watahiniwa 3,272 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa watahiniwa 1,602 (49%) walipata alama 6 hadi 15. Chati Na. 14 inaonesha kwa muhtasari ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.





***Chati Na. 14:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa, asilimia 51 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5, asilimia 46.5 alama 6 hadi 10 na asilimia 2.5 alama 10.5 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 51 walipata alama 0 hadi 5.5. Baadhi yao walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana ya ufundishaji, na hivyo waliandika angalau utangulizi na hoja chache ambazo walishindwa kuzielezea, hivyo walipata alama za chini. Watahiniwa waliopata sifuri (4.3%) hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya *Uendeshaji wa Elimu ya Watu Wazima.* Hivyo waliandika utangulizi usioendana na swali, na pia walitoa hoja zisizohusiana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kuwa wadau hao ni: *wanajamii, sayansi na*

*teknolojia, wataalamu mbalimbali wa elimu, wazazi, wadau wa dini* na *taasisi mbalimbali za kifedha*. Mtahiniwa mwingine alifafanua wadau ambao ni: *Maria Motesori, Paul* na *Siera.* Mtahiniwa mwingine alibaini na kufafanua wadau hao kama vile: *Plato, Sekou toure* na *John Jewey.* Siyo hao tu, mtahiniwa mwingine alibaini na kufafanu wadau kama vile: *baraza la elimu, jamii, watu wazima wote* na *washauri*. Mifano yote hii ni ya majibu ya kukosa; jambo linaloashiria kuwa watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa kuhusu wadau wa elimu ya watu wazima. Kielelezo Na.14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hawakujibu ipasavyo swali la 14.



14 Elimu, ni kitendo cha kupata maarifa,
stadi na mielekeo kutokana na kile ulic
hofundishwa. wafuatao ni wadau wa elim
u ya watu wazima waliotoa mchango wao
katika kuendeleza elimu hiyo nchini Tanza
nia.

Mwalimu Julius Nyerere katika miaka
ya 1970 ndugu mwalimu nyerere alihamasisha
utoaji wa elimu kwa watu wazima ili wawere
kupata maarifa stadi na ujuzi watakaoutu
mia katika maisha.

Rashid mfaume Kawawa pia mheshimi
wa kawawa naye alikuwa na mtazamo
tofauti kuhusiana na suala la elimu ya wa
tu wazima kutokana na kuleta muamko
mkubwa katika suala hili.

Benjamin Mkapa vilevile mkapa alie
ndeleza sera hii ya elimu kwa watu wazima
kutokana na kukuza na kuibua vipaji mb
alimbali katika utendaji.

Edward sokoine, vilevile naye alitoa
mchango wake katika suala zima la kuta
ka kuendeleza elimu ya watu wazima
ambayo itawafanya wawere kuishi vizuri

Ally hassan mwinyi, vilevile katika kuha
kikisha kuwa elimu ya watu wazima inatole
wa waliweka sera mbalimbali ambalo litafa
nikisha uwepo wa elimu hiyo.

John malecela, pia katika kutaka ku
wa na wananchi bora sera hizi ziliendelea ku
wekwa ili kuwezesha watu kupata maarifa.

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alifafanua waliowahi kuwa viongozi wakuu wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, badala ya kufafanua wadau wa elimu ya watu wazima waliotoa mchango wao katika kuendeleza elimu hiyo hapa Tanzania.

Aidha, asilimia 46.5 ya watahiniwa walipata alama 6 hadi 10. Watahiniwa hao walitoa hoja pungufu na baadhi ya maelezo hayakuwa na uhusiano na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua wadau sahihi ambao ni: *serikali* na *shule*. Hoja ya *Wizara ya Elimu* ni marudio ya hoja ya *Serikali*. Aidha, hoja za *jamii*, *wazazi* na *taasisi za elimu* zilikuwa ni dhaifu na hazikustahili kupata alama zote. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya wadau wa elimu ya watu wazima.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 2.5 walipata alama 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao walibaini wadau sahihi wa elimu ya watu wazima waliotoa mchango wao katika kuendeleza elimu hiyo hapa Tanzania. Pia, watahiniwa hao walikuwa na mahiri katika uandishi wa insha tangu utangulizi hadi hitimisho. Baadhi ya watahiniwa walibaini wadau sahihi, lakini hawakutoa maelezo yenye kutosheleza hivo kushindwa kupata alama za juu zaidi. Baadhi ya wadau waliofafanuliwa katika kundi hili ni pamoja na; *mashirika ya kimataifa kama vile UNESCO, NORAD na SIDA, vyuo vya mendeleo, serikali kuu na Serikali za mitaa, chama cha TANU na baadae CCM, baadhi ya vyuo, hasa chuo cha ushirika Moshi, shule za msingi* na *taasisi ya elimu ya watu wazima Tanzania*. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejitahidi kujibu swali hili kwa usahihi.

14. Elimu ya watu wazima ni elimu iliyokuwa ikitolewa kwa watu wenye umri wa miaka 18 nakuendelea ambao hawa kupata elimu kablo ya hapo, Elimu hii pia huweza kutolewa hata kwa wale ambao hawajafikisha miaka 18 kutokana na changamoto ambazo ziliwapata hawakwenda shule. Elimu hii imesaidia watu wengi kupata maarifa juu ya stadi mbalimbali za kazi hata kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Zifuatazo ni hoja zinazoeleza na kuonesha wadau mbalimbali na michango waliyotoa katika kuendeleza elimu ya watu wazima nchini Tanzania. Nao ni kama wafuatao;-

Chuo kikuu cha ushirika; Chuo hichi kinapatikana mkoa wa Kilimanjaro ambapo kilijihusisha na utoaji wa elimu kwa watu wazima katika nchi kwani walitumia vyombo vya mawasiliano mfano redio, runinga na vyombo vingine, lengo lilikua ni kutoa mafunzo kwa watu wote wazima ili kuwajengea mitazamo chanya maishani

Shule; Watu wazima wanaohitaji mafunzo huwa na shule mahalumu yakusoma kwani wao hufundishwa tofauti na watoto wadogo, hivyo kutokana na shule hizo watu wazima wengi wamejitokeza ili wapate elimu hasa kwa wale wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Lakini pia walipata mafunzo ya uongozi, stadi za kazi na mitazamo chanya ambayo iliwajenga.

Vyama vya siasa; Mfano CCM, chama hiki ni chama ambacho kinaongoza nchi kwa sasa lakini kimekua kikiendeleza kwa kiasi kikubwa elimu ya watu wazima kwa kampeni mbalimbali na hata kwa vyombo vya habari ili watu wote hata walio vijijini waweze kutambua umuhimu wa kujifunza au kupata Elimu.

Serikali; Serikali imekua ikitoa fursa za watu wazima kupata mafunzo katika nyanja mbalimbali mfano wale wanaojua kusoma na kuandika

14 Cont.

na hawana elimu ya zaidi wamekuwa wakipewa mafu
nzo mfano kutengeneza sabuni za maji na hata upishi
na ushoni wa nguo jambo ambalo limefanya watu
wengi nchini kujiajiri katika nyanja mahususi.
Vyuo mbalimbali vya maendeleo nchini; Katika vyuo
vikuu vingi nchini vimekuwa vikitoa elimu kwa watu
wazima wanaotaka kujiendeleza zaidi kielimu lakini
pia kwa wale ambao hawakufanikiwa kupata elimu
tangu zamani na Chuo Kikuu cha mwenge kimekua
mfano mzuri katika kutoa elimu hii nchini.
Wataalamu na mashirika binafsi; Mashirika mbali
mbali ya watu binafsi nchini wamekuwa wakitoa
elimu kwa watu wazima katika jamii, watumishi
wa Taasisi hizo pia wamekua wakitoa elimu kwa
watu wazima kwenye jamii zao, jambo ambalo
limeleta mchango mkubwa katika kuendeleza elimu hii.
Hivyo ni vyema na walimu tarajali nao wapa
te elimu hii ili wafikapo katika jamii zao waka
wahamasishe wale ambao hawajapata elimu waweze
kujifunza. Mwalimu tarajali pia anaweza kuwa mo
walimu wa watu wazima katika kusoma, kuandi
ka na kuhesabu.

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na.14.2, mtahiniwa alibaini kwa usahihi wadau wa elimu ya watu wazima waliotoa mchango wao katika kuendeleza elimu hiyo hapa Tanzania. Hata hivyo, baadhi ya hoja hazikutolewa ufafanuzi wenye kujitosheleza.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Kati ya mada 10 zilizotahiniwa katika somo la Ualimu, mada tano (5) zilikuwa na ufaulu mzuri. Mada hizo ni: *Makuzi na Ukuaji wa Mtoto (96.1%), Maendeleo ya Elimu Tanzania (94.7%), Mtaala (89.8%), Uongozi wa Elimu Tanzania (82.5%)* na *Upimaji Katika Elimu (78.2%)*. Kwa upande mwingine mada tatu (3) za *Elimu ya Watu Wazima, Ufundishaji* na *Tathmini Katika Elimu* zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu cha *asilimia 61.9, 57.6* na *50.1* mtawalia. Aidha, mada za *Utafiti wa Kielimu (19.3%)* na *Nadharia za Kujifunza (17%)* zilikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa umewasilishwa katika Kiambatisho cha Pekee.

Ufaulu mzuri kwenye somo hili umesababishwa na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa katika mtihani wa mwaka 2022, isipokuwa mada ya *Utafiti wa Kielimu* na *Nadharia za Kujifunza*.

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2022 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.85 ya watahiniwa walipata asilimia 40 hadi 73.5. Hata hivyo, ufaulu wa mwaka 2022 umeshuka kwa asilimia 0.15 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2021 ambapo asilimia 100 ya watahiniwa walifaulu. Watahiniwa wengi walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa, uwezo mzuri wa kubaini matakwa ya maswali na ujuzi wa kutosha juu ya uandishi sahihi wa insha. Hata hivyo watahiniwa wachache walishindwa kupata alama za juu kwa sababu ya uwezo mdogo wa uandishi na ufafanuzi wa hoja hasa katika maswali ya insha. Sababu nyingine ni kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana mbalimbali zilizoulizwa, hivyo kupelekea kutoa hoja dhaifu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuendeleza kiwango cha ufaulu katika mada zilizofanya vizuri na kuboresha ufaulu katika mada zenye ufaulu wa wastani na hafifu, mambo yafuatayo yanapendekezwa;

(a) Kutumia mbinu ya kazi mradi ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufanya tafiti ndogo wa kielimu kuhusu mada mojawapo ya masuala mtambuko katika elimu. Ni vyema wakufunzi wakaandaa kazi mradi ili walimu tarajali wajifunze zaidi kwa vitendo namna ya kufanya Utafiti wa Kielimu katika mazingira halisi.

(b) Kutumia mbinu ya kisa mafunzo kuhusu namna ya kuandika ripoti ya tathmini ya somo. Wakufunzi wanatakiwa kuwafundisha walimu tarajali kwa kutumia mbinu ya kisa mafunzo na kuwasisitiza kujisomea makala na machapisho yanayohusu mada ya *Tathmini Katika Elimu*. Aidha, mbinu ya kualika mgeni (mwalimu mzoefu) kutoa uzoefu wake kuhusu uandishi wa ripoti ya tathmini ya somo inashauriwa kutumika.

(c) Kutumia mbinu ya utafiti wa maktaba kuhusu uhawilisho wa mafunzo na aina za uhawilisho wa mafunzo. Pia kutumia onesho mbinu na bungua bongo ili kuongeza ufaulu katika mada ya *Nadharia za Kujifunza*.

*Kiambatisho cha pekee*

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ZA SOMO LA UALIMU**

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ufaulu katika kila swali (%) | Wastani wa ufaulu katika kila swali (%) | |
| 1. | Makuzi na Ukuaji wa Mtoto | 11 | 96.1 | 96.1 | Vizuri |
| 2. | Maendeleo ya Elimu Tanzania | 8 | 94.7 | 94.7 | Vizuri |
| 3. | Mtaala | 4 | 89.8 | 89.8 | Vizuri |
| 4. | Uongozi wa Elimu Tanzania | 10 | 82.5 | 82.5 | Vizuri |
| 5. | Upimaji Katika Elimu | 5 | 88.2 | 78.2 | Vizuri |
| | | 13 | 68.1 | | |
| 6. | Elimu ya Watu Wazima | 9 | 74.8 | 61.9 | Wastani |
| | | 14 | 49.0 | | |
| 7. | Ufundishaji | 3 | 16.1 | 57.6 | Wastani |
| | | 12 | 99.1 | | |
| 8. | Tathmini Katika Elimu | 7 | 50.1 | 50.1 | Wastani |
| 9. | Utafiti wa Kielimu | 6 | 36.9 | 19.3 | Hafifu |
| | | 1 | 1.6 | | |
| 10. | Nadharia za Kujifunza | 2 | 17.0 | 17.0 | Hafifu |